# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# BUNGE LA TANZANIA

## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA TATU

## KIKAO CHA AROBAINI NA TISA

**15 JUNI, 2026**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA TATU

### KIKAO CHA AROBAINI NA TISA – TAREHE 15 JUNI, 2026

**I. DUA:**

**II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2025, Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 na Tathmini ya Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 pamoja na Mapendekezo ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

## III. MASWALI:

## OFISI YA WAZIRI MKUU (TAMISEMI):

### 578. MHESHIMIWA ENG. MWANAISHA NG'ANZI ULENGE (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, lini Barabara ya Mwanyungu hadi Chongoleani kunakojengwa Matenki ya Mafuta ya Mradi wa Bomba la Mafuta itajengwa kwa kiwango cha lami.

### 579. MHESHIMIWA BAZILIO KAPUNDA MBWILO (NKASI KASKAZINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itaanza kuwalipa Posho Wenyeviti wa Vijiji na Mitaa.

### 580. MHESHIMIWA TARIMBA GULAM ABBAS (KINONDONI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, Serikali ipo tayari kutoa Waraka wa kurahisisha utoaji wa mikopo ya 10% kutokana na changamoto za Kisheria zinazowakumba walengwa.

**581. MHESHIMIWA ALLY YAHYA MHATA (NANYUMBU):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itadhibiti migogoro ya Wakulima na Wafugaji katika maeneo ya Kata za Sengenya, Lumesore, Mkonona na Masuguru.

**582. MHESHIMIWA ZUENA ATHUMANI BUSHIRI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itatoa kibali cha kubadili matumizi eneo la wazi la Manyema - Moshi kuwa eneo la Soko.

## OFISI YA RAIS (MIPANGO NA UWEKEZAJI):

**583. MHESHIMIWA YOHANA STEPHEN MSITA (ITIGI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Mipango na Uwekezaji):-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kutenga Maeneo Maalum ya Uwekezaji (SEZ) na kuyalipia fidia ili kuvutia Wawekezaji nchini.

## WIZARA YA MAJI:

## 584. MHESHIMIWA FARAJI BURIANI NANDALA (NDANDA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini Serikali itaanza kutekeleza Mradi wa Maji kutoka Mto Ruvuma kupitia Wilaya ya Nanyumbu hadi Jimbo la Ndanda.

## WIZARA YA UCHUKUZI:

## 585. MHESHIMIWA EDIFONSI JOACKIM KANONI (KALAMBO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi:-

Je, lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Meli ya Abiria katika Ziwa Tanganyika.

## 586. MHESHIMIWA HAMOUD ABUU JUMAA (KIBAHA VIJIJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga *Airport* katika Mji wa Kwala ambao ni Mji wa Viwanda na Biashara ili kurahisisha usafiri na kuvutia Wawekezaji.

## WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

### 587. MHESHIMIWA MABULA JOHNSON MAGANGILA (MSALALA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, lini Serikali itajenga Kituo cha Polisi katika Kata ya Bulige.

### 588. MHESHIMIWA DKT. RITTA ENESPHER KABATI (KILOLO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, lini Serikali itawajengea Askari Polisi wa Wilaya ya Kilolo makazi ya kuishi.

## WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:

### 589. MHESHIMIWA MGORE MIRAJI KIGERA (MUSOMA MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum:-

Je, lini Chuo cha Maendeleo ya Jamii Buhare kitapandishwa hadhi kutoa Shahada badala ya ngazi ya Cheti na Stashahada kwa miaka 58.

**WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:**

**590. MHESHIMIWA ERIC JAMES SHIGONGO (BUCHOSA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, lini Serikali itafanya sensa ya Mamba na kuwavuna kwa kuwa Wananchi wanapoteza uhai kwa kuliwa na Mamba.

**591. MHESHIMIWA FLORENT LAURENT KYOMBO (MISSENYI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, lini Serikali itawapa Wananchi wa Missenyi Hekta 2000 kati ya Hekta 9000 za eneo la Msitu wa Bushenya kama walivyoomba.

**IV. HOJA ZA SERIKALI:**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MIPANGO NA UWEKEZAJI):**

Kwamba Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2025 na

Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

**WAZIRI WA FEDHA:**

Kwamba Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

***(Majadiliano yanaendelea)***

**DODOMA**
**15 JUNI, 2026**

**BARAKA I. LEONARD**
**KATIBU WA BUNGE**